JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS – TAMISEMI

FOMU YA KUJIUNGA NA SHULE

SHULE YA SEKONDARI AYALAGAYA

S.L.P 267,

BABATI.

Kumb. Na. ASS/JI/VOL.16

MAWASILIANO

SIMU Na. 0765-793 763

0692 -670 778

JINA LA MWANAFUNZI …….

YAH: MAAGIZO YA KUJUINGA NA SHULE YA SEKONDARI AYALAGAYA KIDATO CHA TANO 2022/2023.

1.0 UTANGULIZI

Ninayo furaha kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule ya sekondari Ayalagaya mwaka 2022. **Hongera sana.**

Shule hii ni ya kutwa kwa kidato cha kwanza hadi kidato cha nne na bweni kwa kidato cha tano na sita. Shule ipo katika Kijiji cha Dareda Kati Kata ya Ayalagaya, Tarafa ya Bashneti, Wilaya ya Babati mkoa wa Manyara. Kwa wanafunzi wanaotokea Dar es salaam, Pwani Tanga, Arusha na mikoa ya jirani ukifika Babati mjini tafuta magari yanayoenda Dareda centre na ushukie hapo na ulizia shule ya sekondari Ayalagaya. Kwa wanaotokea kanda ya ziwa, kanda ya magharibi, nyanda za juu kupitia Singida washukie dareda centre halafu ulizia shule ya sekondari Ayalagaya ambayo ipo mita 100 kutoka stendi ndogo ya dareda centre. Shule iko umbali wa kilometa 25 magharibi mwa makao makuu ya Mkoa/Halmashauri ya Wilaya ya Babati.

1.1 Shule itafunguliwa muhula wa kwanza wa masomo kwa tarehe rasmi itakayotangazwa na serikali. unatakiwa kuripoti shuleni tarehe ya kufungua shule bila kukosa, nje na hapo hutapokelewa. Aidha mzazi/mlezi wa mwanafunzi lazima umlete mwanao siku ya kuripoti shuleni akiwa na mahitaji yote yaliyoagizwa, mwanafunzi hatapokelewa bila ya mzazi/mlezi

2.0 MAHITAJI MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1 SARE ZA SHULE

Unatakiwa kuja na sare za shule kama ifuatavyo:-

A. KWA WAVULANA

i) Suruali mbili ya rangi **"dark blue"** kitambaa kizito namba moja, yenye mifuko miwili pembeni, mmoja nyuma na mkunjo kwa chini (turn up) isiwe na mshono wa jinsi.
ii) Shati mbili za rangi nyeupe aina ya tetron mikono mirefu
iii) Sweta mbili za rangi ya "**dark blue"** yenye nembo ya robin isiwe ya mgongesho.
iv) Soksi jozi mbili rangi nyeusi:.
v) Fulana (T –shirt nyeupe ya ndani)
vi) Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba jozi mbili
vii) Mkanda mmoja mweusi wa Ngozi usiwe na madoido yoyote.
viii) Picha mbili passpot size, ukiwa umevaa sare ya shule
ix) Vifaa vya usafi – Hardbroom moja, ndoo ndogo mbili, soft broom moja, squizer moja jembe moja na ufagio wa chelewa mmoja.
x) Rimu mbili A4 kwa ajili ya mitihani na mazoezi.
xi) Godoro futi 2.5 upana
xii) Tranka moja lakuhifadhia nguo na vifaa vingine muhimu
xiii) Shuka mbili rangi ya pink
xiv) Blanket moja
xv) Tracksuit nyeusi yenye mistari meupe
xvi) T-shirt yenye nemmbo ya shule, inapatikana shuleni kwa 15,000/=

B. KWA WASICHANA

i) Sketi mbili za rangi ya **"dark blue"** kitambaa kizito namba moja. Sketi ziwe ndefu na marinda yawe nane (8) yaani mbele 04 na nyuma 04.
ii) Shati mbili za rangi nyeupe aina ya tetron mikono mifupi
iii) Sweta mbili za rangi ya "**dark blue**" nembo ya robin isiwe ya mgongesho.
iv) Soksi ndefu (stocking) jozi mbili rangi nyeupe
v) Viatu vyeusi vya kufunga na kamba jozi mbili visiwe na visigino virefu.
vi) Wanafunzi wa kiislamu wanaruhusiwa kuvaa shungi rangi nyeupe usiwe na urembo wa aina yoyote (tumia kitambaa cheupe aina ya tetron).
vii) Picha mbili za passport size zikiwa umevaa sare ya shule
viii) Vifaa vya usafi – Hard broom moja, soft broom moja, squizer moja, ndoo ndogo moja jembe moja na ufagio wa chelewa.
ix) Rimu mbili ya A4 kwa ajili ya mitihani na mazoezi.
x) Hairuhusiwi kusuka wala kuweka kucha rangi.
xi) Godoro moja 2.5ftx3x6
xii) Tranka moja lakuhifadhia nguo na vifaa vingine muhimu
xiii) Shuka mbili rangi ya pink
xiv) Blanket moja
xv) Tracksuit nyeusi yenye mistari meupe
xvi) T-shirt yenye nemmbo ya shule, inapatikana shuleni kwa 15,000/=

C. NGUO ZA MICHEZO (KWA WOTE)

i) Raba jozi moja nyeusi kwa wasichana na njumu kwa wavulana
ii) Fulana (T –shirt) moja rangi ya ugoro zinapatikana shuleni.
iii) Bukta moja rangi nyeusi kwa wavulana
iv) Sketi moja rangi nyeusi kwa wasichana

N.B Uvaaji wa sare za shule ni muhimu na ni lazima uwe na sare zenye heshima. Suruali za kubana (mnyonyo) au mashono mfumo wa jinsi, sketi fupi, hazitaruhusiwa kabisa shuleni.

Aidha mwanafunzi anatakiwa kuja na fomu ya kujiunga na shule, fomu ya Daktari zote ziliwa zimejazwa na wahusika siku ya kuripoti shuleni.

2.2 MAAGIZO MENGINE

A. VIFAA VYA MADARASANI

i) Madaftari makubwa yasiyopungua kumi na mbili (12) (counter book quire 3)
ii) Kalamu za wino za kutosha nyeusi au bluu
iii) Mkebe wa hisabati (mathematical set)
iv) Faili moja kwa ajili ya kutunza (kuhifadhia) kumbukumbu zake shuleni.
v) Begi imara la kubebea madaftari vifaa vyake vingine.
vi) Vitabu binafsi vya ziada kulingana na tahasusi anayosoma mwanafunzi
vii) Dissecting kit kwa tahasusi ya PCB
viii) Scientific calculator kwa wanafunzi wanaosoma Tahasusi ya PCB

B. MICHANGO YA SHULE

Aina ya mchango	kiasi
Ada kwa mwaka	70,000/=
Uboreshaji wa taaluma kwa mwaka	30,000/=
Ulinzi, wahudumu wa ofisi na wapishi kwa mwaka	30,000/=
Mock examination	20,000/=
Joint examination	10,000/=
Tahadhari	5,000/=
ukarabati wa samani	10,000/=
usafiri wa kupeleka wanafunzi wagonjwa hosptalini	10,000/=

N.B fedha zote zilipwe benki NMB account number **4071200100 jina AYALAGAYA SEC RECURRENT**

SHERIA NA KANUNI ZA SHULE HII

2.3 Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo inayotolewa na Wizara ya Elimu na mafunzo ya ufundi Sayansi na Teknologia, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais –TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuwa vizuri mara baada ya kuripoti shuleni.

a) Heshima kwa viongozi,wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wenzake na jamii kwa ujumla ni jambo l lazima.
b) Mahusiano mazuri katika kila shughuli ya ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)

d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kkuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotkiwa
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
i) Kutunza mali za umma.

2:4 KWA MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUKUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE.

a) Wizi
b) Uasheratina ushoga.
c) Ubakaji.
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa bangi, cocaine,mirungi,kuberi na mengineyo.
e) Kupigana au kupiga
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
g) Kudharau bendera ya Taifa.
h) Kupata mimba au kusababisha
i) Kuoa au kuolewa
j) Kutoa mimba
k) Kugoma,kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
l) Kukataa adhabu kwa makusudi.
m) Kuwa na simu ya mkononi shuleni.
n) Utoro wa siku zaidi ya tisini (90) mfululizo bila sababu maalumu.
o) Vilabu vya pombe, nyumba za kufikia wageni,kumbi za starehe n.k.

N.B Adhabu kwa uvunjaji wa sheri za shule zilizotolewa na walimu, baraza la wanafunzi/kamati ya nidhamu.

-Bodi ya shule au vyombo vingine vinavyohusika kisheria na taratibu za nchi.

3.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA WANAFUNZI.

a) Fomu ya Hospitali ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya serikali..
b) Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutokushiriki katika migomo,fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria,kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
d) Fika na fomu hii shuleni kama kitambulisho chako.

UNAKARIBISHWA KATIKA SHULE YA SEKONDARI AYALAGAYA.

…….
MKUU WA SHULE.

FOMU YA TAARIFA MAALUM KUHUSU MWANAFUNZI

(Taarifa zote zijazwe kwa herufi kubwa)

SEHEMU A:

Jina kamili ……..

Tarehe ya kuzaliwa …… Kabila ……... Dini …….....

Jina la Mzazi/Mlezi …….

Anwani ya Nyumba …….

Kijiji ……. Kata …… Tarafa……...

Wilaya ……. Mkoa ……..

SEHEMU B:

Kazi ya wazazi/Mlezi …….

Namba ya simu ya Mzazi/Mlezi ……..

SEHEMU C:

Mambo ambayo unapendelea kufanya baada ya muda wa masomo (kama Michezo,Bustani,Kushona).

(1)…….....(2) ……..(3)…… (4) ……

SEHEMU D:

Ndugu na jamaa (Kufuata umri wao)

Majina ya Ndugu	Umri	Kiwango cha Elimu	Anwani	Simu

Naahidi kuwa na tabia nzuri mchapakazi na mwenye bidii katika maasomo

Sahihi ya Mwanafunzi……..

Sahihi ya Mzazi/Mlezi …….

Tarehe ……...

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

SHULE YA SEKONDARI AYALAGAYA

FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA SHULE NA MASHARTI YAKE.

Fomu hii irudishwe Shuleni siku ya kuripoti mwanafunzi ikiwa imejazwa kikamilifu.

1. **A: MWANAFUNZI**

   Mimi …… nimesoma kwa makini maagizo ya kujiunga na shule hii, Pia sheria za Shule.Kwa heshima na unyenyekevu mkubwa ninakubali/nimeikataa nafasi hiyo pamoja na masharti na sheria za shule kwa sababu:-

   ……
   ……
   ……
   ……..
   Tarehe ……. Sahihi ……

2. **B: MZAZI/MLEZI**

   Mimi …….. Mzazi/mlezi wa ……
   Ambaye amechaguliwa kujiunga na shule hii, nimesoma maagizo na sheria zake. Ninakubali/ninaikataa nafasi hiyo, ninaahidi/siahidi kumtimizia mtoto wangu mahitaji na maagizo yote ya kujiunga na shule kwa muda wote uliopangwa.
   Aidha, naahidi kushirikiana na uongozi wa shule katika kumkuza, kumlea mtoto huyu kwa manufaa yake binafsi, wazazi na Taifa kwa ujumla.
   Kama unakataa eleza sababu:-

   ……
   ……
   ……....

   Ahsante,
   Jina na anwani ya Mzazi/mlezi ……..
   Tarehe …….. Sahihi ……
   Futa lisilohusika.

   NB: SEHEMU “B” ISAINIWE NA MZAZI/MLEZI NA SI VINGINEVYO.

THE PRESIDENT OFFICE – RALG
MINISTRY OF EDUCATION SCIENCE AND TECHNOLOGY
BABATI DISTRICT COUNCIL
AYALAGAYA SECCONDARY SCHOOL

MEDICAL EXAMINATION FORM – For Joining Secondary Education.

To be completed by government Medical Officer and returned to school on Registration by the Parent/guardian

Students full name …….

Age ……..

Please examine the above mentioned student for the following:-

Blood count (red and white) …….

Stool examination …….

Syphilis …….

T.B Test ……

Eye Test ……

Venereal diseases ……..

Leprosy …….

Ears Test ……...

Spleen ……

Abdomen ……...

Urine …….

Epilepsy ……

Pregnancy Test (for ladies) ……..

Additional information: eg. Physical defect impairment (s) infections chronic or family diseases e.t.c

……
……
……
……

MEDICAL CERTIFICATION (to be completed by the medical Officer)

I have examined the above mentioned student: He/she is fit/unfit to pursue his/her studies for the full time of his/her course at school.

Signature …… **Designation ……..**

Station …… **Date ……..**

OFFICIAL STAMP

NOTE: Medical Officer at the Examination, treat the student for any problem you note.